

KUMB: PPR/18 - 09/1

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 5 SEPTEMBER 2018

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika **Jumatano, Tarehe 5 Septemba 2018**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchini, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote (yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa) yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 1 Agosti 2018. Kwa mwezi Septemba 2018, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 10/lita (sawa na asilimia 0.43), Shilingi 19/lita (sawa na asilimia 0.83) na Shilingi 24/lita (sawa na asilimia 1.05), mtawalia. Vilevile, ukilinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa nazo zimepungua kama ifuatavyo; Shilingi 10.10/lita (sawa na asilimia 0.45), Shilingi 18.95/lita (sawa na asilimia 0.87) na Shilingi 23.78/lita (sawa na asilimia 1.11), mtawalia. Mabadiliko haya ya bei yanatokana na kupungua kwa bei za mafuta kwenye soko la dunia mwezi Julai 2018 ikilinganishwa na zile bei za mwezi Juni 2018 zilizotumika katika bei kikomo za petroli zilizotangazwa mwezi Agosti 2018.
- (b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli katika mkoa wa Tanga zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 1 Agosti 2018. Ifahamike kuwa, kabla ya mwezi Agosti 2018, shehena ya mwisho ya mafuta ya Petroli na Dizeli katika bandari ya Tanga ilipokelewa mwezi Mei 2018. Kwa mwezi Septemba 2018, bei za rejareja za Petroli na Dizeli kwa **Mikoa ya Kaskazini** zimeongezeka kwa Shilingi 114/lita (sawa na asilimia 5.11) na Shilingi 102/lita (sawa na asilimia 4.70), mtawalia. Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 113.70/lita (sawa na asilimia 5.39) na Shilingi 101.50/lita (sawa na asilimia 4.97), mtawalia. Ongezeko la bei za mafuta mkoani Tanga limetokana na ongezeko la bei za mafuta hayo katika soko la dunia kwa mwezi Julai 2018 ikilinganishwa na zile za mwezi Machi 2018, zilizokuwa zikitumika tangu shehena ya mwisho kupokelewa katika bandari ya Tanga.
- (c) Ni vyema ikatambulika kuwa, wakati shehena ya mwisho ya Mafuta ya Taa ilipokelewa katika bandari ya Tanga mwezi Oktoba 2017, kutoptaka na ghala la kuhifadhia mafuta lililopo Tanga kuishiwa mafuta hayo, kuanzia mwezi Aprili 2018, Mikoa ya Kaskazini ilikuwa inapata Mafuta ya Taa kutoka katika ghala za mafuta za Dar es Salaam. Hivyo, bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa Mikoa ya Kaskazini zilitokana na gharama za mafuta hayo yaliyopokelewa katika bandari ya Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika. Ikilinganishwa na bei za Mafuta ya Taa za Dar es Salaam zilizotangazwa katika toleo la mwezi Agosti 2018, bei za mafuta hayo katika Mikoa ya Kaskazini kwa mawezi Septemba 2018 zimepungua kwa asilimia moja kutoptaka na kupungua kwa bei ya mafuta katika soko la dunia.
- (d) Vilevile, kwakuwa hakuna shehena ya mafuta iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Mtwara katika mwezi wa Agosti 2018, bei za mafuta ya Petroli na Dizeli kwa mkoa wa

Mtwara zitaendelea kuwa kama zilivyokuwa mwezi Agosti 2018. Shehena ya mwisho ya mafuta ilipokelewa katika bandari ya Mtwara mwezi Juni 2018 ikiwa imenunuliwa kwa bei ya soko la dunia ya mwezi Mei 2018. Kutokana na kuwepo kwa mafuta mengi katika maghala ya kuhifadhi mafuta Mtwara, bei za mafuta kwa mikoa ya Lindi na Ruvuma zimekokotolewa kutokana na gharama za mafuta kutoka Mtwara. Hivyo, wamiliki wa vituo vyta mafuta katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Mtwara. Kwakuwa hakuna Mafuta ya Taa yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vyta mafuta katika mikoa tajwa wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zitatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.

- (e) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za kiganjani kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuza ya bidhaa za mafuta.
- (g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 269/2018 la mwezi Juni 2018**.
- (h) Vituo vyote vyta mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vyta biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuza wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuza wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mafuta ya petroli.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Dar es Salaam	2,373	2,273	2,247

Arusha	2,405	2,326	2,282
Arumeru (Usa West)	2,405	2,326	2,282
Karatu	2,423	2,345	2,300
Longido	2,416	2,337	2,293
Monduli	2,410	2,332	2,287
Monduli-Makuyuni	2,415	2,336	2,292
Ngorongoro (Loliondo)	2,489	2,411	2,366
Pwani (Kibaha)	2,378	2,277	2,251
Bagamoyo	2,385	2,284	2,258
Chalinze Junction	2,388	2,287	2,261
Chalinze (Msata)	2,392	2,291	2,265
Kibiti	2,394	2,293	2,267
Kisarawe	2,381	2,280	2,254
Mkuranga	2,383	2,282	2,257
Rufiji	2,401	2,300	2,274
Dodoma	2,432	2,331	2,306
Bahi	2,440	2,339	2,313
Chamwino	2,428	2,327	2,301
Chemba	2,459	2,358	2,332
Kondoa	2,465	2,364	2,338
Kongwa	2,430	2,329	2,303
Mpwapwa	2,433	2,332	2,307
Mtera (Makatopora)	2,451	2,350	2,324
Geita	2,539	2,438	2,412
Bukombe	2,528	2,427	2,401
Chato	2,560	2,459	2,433
Mbogwe	2,577	2,476	2,450
Nyang'hwale	2,554	2,453	2,427
Iringa	2,438	2,337	2,311
Ismani	2,443	2,342	2,316
Kilolo	2,442	2,341	2,315
Mufindi (Mafinga)	2,448	2,347	2,321
Kagera (Bukoba)	2,589	2,488	2,462
Biharamulo	2,563	2,462	2,437
Karagwe (Kayanga)	2,605	2,505	2,479
Kyerwa (Ruberwa)	2,611	2,510	2,484
Muleba	2,589	2,488	2,462
Ngara	2,577	2,476	2,450
Misenyi	2,597	2,497	2,471
Katavi (Mpanda)	2,582	2,481	2,455
Mlele (Inyonga)	2,563	2,462	2,437
Mpimbwe (Majimoto)	2,574	2,473	2,447
Kigoma	2,605	2,504	2,478
Uvinza (Lugufu)	2,617	2,516	2,491
Buhigwe	2,594	2,493	2,467
Kakonko	2,562	2,461	2,435
Kasulu	2,591	2,490	2,464
Kibondo	2,569	2,468	2,443

Kilimanjaro (Moshi)	2,394	2,316	2,271
Hai (Bomang'ombe)	2,398	2,319	2,275
Mwanga	2,387	2,309	2,264
Rombo (Mkuu)	2,411	2,333	2,288
Same	2,381	2,302	2,258
Siha (Sanya Juu)	2,401	2,322	2,278
Lindi	2,400	2,373	2,306
Lindi-Mtama	2,405	2,378	2,324
Kilwa Masoko	2,424	2,397	2,281
Liwale	2,436	2,409	2,327
Nachingwea	2,420	2,393	2,335
Ruangwa	2,427	2,400	2,337
Manyara (Babati)	2,439	2,360	2,316
Hanang (Katesh)	2,449	2,371	2,326
Kiteto (Kibaya)	2,454	2,376	2,331
Mbulu	2,451	2,373	2,329
Simanjiro (Orkasumet)	2,471	2,392	2,348
Mara (Musoma)	2,552	2,451	2,425
Musoma Vijijini (Busekela)	2,593	2,492	2,466
Rorya (Ingirijuu)	2,561	2,460	2,434
Rorya (Shirati)	2,596	2,495	2,469
Bunda	2,543	2,442	2,417
Butiama	2,549	2,448	2,422
Serengeti (Mugumu)	2,598	2,497	2,471
Tarime	2,563	2,462	2,436
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,568	2,467	2,441
Mbeya	2,481	2,380	2,354
Chunya	2,490	2,389	2,363
Chunya (Makongolosi)	2,504	2,403	2,378
Kyela	2,496	2,395	2,370
Mbarali (Rujewa)	2,465	2,364	2,338
Rungwe (Tukuyu)	2,490	2,389	2,363
Morogoro	2,398	2,298	2,272
Mikumi	2,414	2,313	2,287
Kilombero (Ifakara)	2,436	2,335	2,310
Kilombero (Mlimba)	2,459	2,358	2,332
Kilombero (Mngeta)	2,448	2,347	2,321
Ulanga (Mahenge)	2,447	2,346	2,320
Malinyi	2,457	2,356	2,331
Kilosa	2,417	2,316	2,290
Gairo	2,417	2,316	2,290
Mvomero (Wami Sokoine)	2,409	2,308	2,282
Turiani	2,424	2,323	2,297
Mtwara	2,387	2,360	2,319
Nanyumbu (Mangaka)	2,423	2,396	2,368
Masasi	2,403	2,376	2,345
Newala	2,408	2,381	2,351
Tandahimba	2,401	2,374	2,344

Nanyamba	2,401	2,374	2,344
Mwanza	2,524	2,423	2,397
Kwimba	2,542	2,441	2,415
Magu	2,532	2,431	2,405
Misungwi	2,518	2,417	2,391
Sengerema	2,556	2,455	2,429
Ukerewe	2,583	2,482	2,456
Njombe	2,466	2,365	2,339
Njombe (Kidegembye)	2,487	2,386	2,360
Ludewa	2,504	2,403	2,377
Makambako	2,458	2,357	2,332
Makete	2,497	2,396	2,370
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,464	2,363	2,337
Rukwa (Sumbawanga)	2,546	2,446	2,420
Sumbawanga Rural (Mtownisa)	2,546	2,446	2,420
Kalambo (Matai)	2,554	2,453	2,427
Nkasi (Namanyele)	2,560	2,459	2,433
Ruvuma (Songea)	2,472	2,445	2,370
Mbinga	2,485	2,458	2,404
Namtumbo	2,463	2,436	2,400
Nyasa (Mbamba Bay)	2,510	2,483	2,406
Tunduru	2,438	2,411	2,429
Shinyanga	2,502	2,401	2,376
Kahama	2,516	2,415	2,389
Kishapu	2,531	2,430	2,404
Ushetu (Nyamilangano)	2,534	2,433	2,407
Simiyu (Bariadi)	2,544	2,443	2,417
Busega (Nyashimo)	2,537	2,436	2,410
Itilima (Lagangabilili)	2,547	2,446	2,420
Maswa	2,535	2,434	2,409
Meatu (Mwanhuzi)	2,542	2,441	2,416
Singida	2,464	2,363	2,338
Iramba	2,476	2,375	2,350
Manyoni	2,449	2,348	2,322
Ikungi	2,460	2,359	2,333
Mkalama (Nduguti)	2,489	2,388	2,362
Songwe (Vwawa)	2,490	2,389	2,363
Songwe (Mkwajuni)	2,497	2,396	2,370
Ileje	2,494	2,393	2,367
Momba (Chitete)	2,499	2,398	2,372
Tunduma	2,494	2,393	2,367
Tabora	2,528	2,427	2,401
Igunga	2,482	2,381	2,355
Kaliua	2,547	2,446	2,420
Ulyankulu	2,541	2,440	2,414
Nzega	2,492	2,391	2,366
Sikonge	2,540	2,439	2,413
Urambo	2,541	2,440	2,414

Uyui	2,529	2,428	2,402
Tanga	2,348	2,270	2,225
Handeni	2,369	2,290	2,246
Kilindi	2,384	2,305	2,261
Korogwe	2,360	2,282	2,237
Lushoto	2,369	2,291	2,247
Mkinga (Maramba)	2,355	2,277	2,232
Muheza	2,353	2,274	2,230
Pangani	2,355	2,276	2,232

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,249.05	2,148.04	2,123.00

Bei za Jumla - TANGA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,223.62	2,145.19	2,101.39

Bei za Jumla - MTWARA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,262.35	2,235.07	---

Nzinyangwa E. Mchany
KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA